

# Ruvuma: Uandishi wa habari wakwazwa

## WANAHABARI WATUMIKA KUKANUSHA HABARI YA MWANDISHI MWENZAO

# Ruvuma: Uandishi wa habari wakwazwa

## WANAHABARI WATUMIKA KUKANUSHA HABARI YA MWANDISHI MWENZAO

Media Council of Tanzania (MCT)
P.O Box 10160, Dar es Salaam, Tanzania.

**Ruvuma: Uandishi wa habari wakwazwa**

©Media Council of Tanzania (MCT)  2019

ISBN   978-9987-710-75-1



*Wanafunzi wakiwa kwenye darasa lililoezekwa kwa nyasi katika shule ya Msingi ya Ulamboni katika kata ya Kizuka katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea, mkoa wa Ruvuma.Hata hivyo maofisa wa Serikali wanadai kuwa hilo si darasa bali ni mahala wanafunzi hutumia kwa kunywa uji.*

## MAELEZO YA PICHA YA JALADA:

*Daraja la kienyeji katika kijiji cha Mipeta, kata ya Muhukuru katika Halamashauri ya Songea linalounghanisha eneo hilo na Wilaya ya Mbinga ambako wananchi huenda kufuata matibabu katika kituo cha Afya cha Kalembo.*

# YALIYOMO


SHUKRANI ....................................................................................................5

1.0: UTANGULIZI ....................................................................................................6

2.0: CHIMBUKO ....................................................................................................7

3.0: HADIDU ZA REJEA ZA UCHUNGUZI ..........................................................7

4.0: TARATIBU ZA UCHUNGUZI ....................................................................8

5.0: UCHUNGUZI WA SONGEA ......................................................................8

6.0: TAARIFA ZA WAHUSIKA MMOJA MMOJA: ..........................................11

7.0: HITIMISHO ....................................................................................................25

8.0: MAPENDEKEZO: ..........................................................................................27

10.0: VIAMBATANISHO ....................................................................................28

## SHUKRANI:

Ripoti hii ni matokeo ya juhudi zilizoratibiwa na Sekretarieti ya Baraza la Habari Tanzania (MCT), wachunguzi, wanahabari walio wanachama wa Klabu ya Waandishi wa Habari ya Ruvuma, uongozi wa wilaya Songea na mkoa wa Ruvuma na wadau wengine ambao kwa pamoja wamewezesha kazi hii kufanyika.

Timu ya uchunguzi ilijumuisha Kiongozi wa Timu Hamis Mzee – Mhariri kutoka Baraza la Habari Tanzania, na wajumbe: Florence Majani, ofisa wa Sera ya Vyombo vya Habari, Programu na Ushauri kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), na Lucas Liganga, Mhariri Mshiriki kutoka Kampuni ya The Guardian.

MCT inatoa shukrani za dhati kwa wajumbe wa timu kwa kutoa muda wao muhimu na wadau wote kwa majibu, maoni na mapendekezo yao katika kufanikisha kazi hii.

# 1.0 UTANGULIZI

1.1 Mnamo Oktoba 12, 2018, Geofrey Nilahi, mwandishi wa habari mwenye makazi yake Songea, Mkoani Ruvuma, aliandika barua pepe kwa MCT, akiliarifu Baraza juu ya vitisho dhidi yake kutoka kwa maofisa wa Serikali mkoani humo. Nilahi ni mwandishi wa kujitegemea kwenye vyombo viwili vya habari vilivyopo jijini Dar es Salaam: Channel 10 na gazeti la Tanzania Daima.

Mwandishi huyo alidai kwamba vitisho hivyo vilitokana na taarifa yake juu ya hali mbaya ya shule kwenye maeneo ya vijiji vya Mipeta na Lunyele kwenye Kata ya Muhukuru. Alitembelea vijiji hivyo mnamo Septemba 26, 2018 kufuatia kudokezwa kwamba wakazi wa maeneo hayo walikuwa wanakabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwemo hali mbaya ya barabara na zahanati isiyofanya kazi.

Vile vile, Shule ya Msingi ya Muungano kwenye eneo hilo ilikuwa imefungwa kutokana na ukosefu wa walimu na madarasa yalikuwa kwenye hali mbaya sana. Mbali na hayo, kulikuwepo na madaraja yaliyovunjika. Kurushwa hewani na kuchapishwa kwa taarifa hizo kulizusha mjadala miongoni mwa wananchi kupitia mitandao ya kijami. Hali hiyo iliwafadhaisha viongozi mkoani Ruvuma ambao waliona ni wajibu wao kutembelea maeneo husika kwa nyakati tofauti.

Nilahi alilieleza Baraza kwamba kufuatia taarifa yake hiyo, Christina Mndeme, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, alimuita ofisini kwake na kumueleza kwamba alikuwa ametakiwa na Mwenyekiti wa Taifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kueleza ni kwanini alimruhusu mwandishi wa habari kuandika taarifa ambayo ilikuwa inatoa picha mbaya kwa chama tawala.

Mwandishi huyo alitakiwa kuelezea taarifa yake hiyo. Pia, viongozi wa mkoa wa Ruvuma na wale wa Wilaya ya Songea walimshutumu kwa kuchafua taswira ya Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho.

Maofisa hao walimshutumu Nilahi kwa kuweka uzito wa taarifa yake kwenye masuala hasi huku akipuuza yale ambayo ni chanya. Lakini mwandishi huyo, kwenye utetezi wake, alisema kwamba alikuwa amejaribu kuwasiliana na Mheshimiwa Mhagama kwa simu na ujumbe wa mfupi wa simu ili kuweka uwiano kwenye habari hiyo, lakini hakufanikiwa, kwa vile kiongozi huyo alikuwa hapatikani kwa muda wote aliomtafuta.

Nilahi alisema kwamba baada ya majibizano hayo na viongozi wa mkoa wa Ruvuma, kama hatua ya kujibu mapigo, waliwapa kazi waandishi kutoka vyombo vya habari shindani kuchapisha na kurusha habari zinazopingana na taarifa zake juu ya hali ya shule kwenye Wilaya ya Songea. Alitaja baadhi ya vyombo vya habari vilivyotoa habari hizo za kupinga taarifa yake, kuwa ni gazeti la Majira, Azam TV, Star TV na magazeti ya Kampuni ya Mwananchi.

Mwandishi huyo alihofia usalama wake na kuamua kutoa taarifa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) wa Songea. Hata hivyo, mkuu huyo wa polisi alimpuuza, akisema kwamba vitisho hivyo havikuwa vya kweli na vilikuwa vinafanywa na wahuni. Ibara 3 (e) ya Katiba ya MCT inataka Baraza kuwa na taarifa kimandishi za matukio yanayoweza kuzuia upatikanaji wa taarifa zenye manufaa na umuhimu kwa jamii, kuweka muendelezo wa mara kwa mara wa matukio hayo, na kuchunguza tabia na mienendo ya watu, makampuni na taasisi za serikali katika ngazi mbalimbali, kwa vyombo vya habari na kuweka bayana kwa umma matokeo ya uchunguzi huo.

MCT iliunda timu ya wajumbe watatu kufuatilia na kuchunguza madai ya Nilahi. Timu hiyo ililenga kubainisha kama utoaji taarifa wa mwandishi huyo ulikuwa wa haki na kama alipokea vitisho kutoka kwenye mamlaka za mkoa kufuatia taarifa zake. Uchunguzi huo ulitakiwa kubaini kama kulikuwepo na ukiukwaji wowote wa uhuru wa vyombo vya habari na kutoa mapendekezo kwa Baraza.

## 2.0: CHIMBUKO

2.1 Vyombo vyote vikubwa vya habari nchini Tanzania vina wawakilishi mkoani Ruvuma. Vyombo hivyo vya habari na magazeti vyenye wawakilishi au waandishi wa kujitegemea mkoani humo ni pamoja na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), MCL, Majira, Tanzania Daima, Habari Leo, Nipashe, Redio One, Redio Free Africa, Azam TV, Channel 10 na Star TV. Vile vile kuna Key FM na Jogoo FM, zote zikiwa na makao makuu yao Songea.

Kuna takriban waandishi wa habari 80 mkoani Ruvuma na 38 kati yao ni wanachama wa RPC. Na 15 kati ya wanachama hao 38 wa RPC ni waandishi wanaofanyakazi hiyo huku wengine waliobakia wakiwa hawafanyi kazi hiyo kwa sasa.

## 3.0: HADIDU ZA REJEA ZA UCHUNGUZI

3.1: Hadidu za rejea zilikuwa:

(i) Kubaini nini kilichotokea mnamo Septemba 26, 2018 kwenye Wilaya ya Songea, Mkoani Ruvuma kuhusiana na mwandishi wa habari aliyekuwa anashughulikia taarifa juu ya kufungwa kwa Shule ya Msingi ya Muungano iliyopo Wilaya ya Songea;

(ii) Kutathmini kama mwandishi huyo alitishiwa, na nani na kwa sababu gani;

(iii) Kuchunguza uhusiano kati ya wafanyakazi wa vyombo vya habari Mkoani Ruvuma na vyanzo vyao vya habari pamoja na uhusiano kati yao na mamlaka za wilaya na mkoa;.

(iv) Kuchunguza ukiukwaji mwingine wa uhuru wa vyombo vya habari, kama upo, ambao unaandamana na kazi na usalama wa waandishi wa habari Mkoani Ruvuma;

(v) Kuulizia mazingira ya kazi kwa ujumla ya waandishi wa habari Mkoani Ruvuma na kuangalia kama kuna viashiria vya hatari vinavyowakabili wakati wakifanya kazi zao na kutoa mapendekezo;
(vi) Kupendekeza muendelezo na utaratibu wa ulinzi na au hatua za kurekebisha ambazo zinaweza kuchukuliwa na Baraza na washirika wake
(vii) Kufanyakazi kwenye timu ya washauri watatu kwa ushirikiano na Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari ya Ruvuma katika utekelezaji wa kazi hiyo.
(viii) Kuandaa taarifa inayoweka bayana yaliyomo kwenye uchunguzi huo pamoja na kutoa mapendekezo kwa hatua ya kuchukuliwa na MCT na washirika wake na;
(ix) Kuhakikisha Baraza linataarifiwa kikamilifu maendeleo ya jopo hilo na kulitaarifu Baraza mara moja pale panapoibuka hali ambayo inaweza kuhatarisha kufanikiwa kwa utekelezaji wa jukumu hilo.

## 4.0: TARATIBU ZA UCHUNGUZI

4.1. Timu ya uchunguzi ilipata sehemu kubwa ya taarifa zake kupitia njia ya mahojiano na mwandishi aliyedai kuwa muhanga, Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Ruvuma, waandishi waliopo Songea na mamlaka za mkoa wa Ruvuma. Timu hiyo pia ilitumia taarifa za magazeti, video na taarifa zilizohusiana na tukio hilo.

## 5.0: UCHUNGUZI WA SONGEA

**KWA UJUMLA:**

Sekretarieti ya MCT ilipata lalamiko adimu kutoka kwa mwaandishi mwenye makazi yake Wilayani Songea katika Mkoa wa Ruvuma, akiwatuhumu waandishi wenzake kurubuniwa na viongozi wa wilaya na mkoa ili kukanusha habari yake ya uchunguzi iliyoelezea uwepo wa daraja bovu na hatari, vyumba vya madarasa chakavu na zahanati isiyofaa kutoa huduma katika vijiji vya Mipeta, Lunyele na Muhukuru Wilayani Songea.

MCT ilituma timu kwenda Wilayani Songea mnamo Novemba 10, 2018 kuchunguza lalamiko hilo. Tukio hilo linaangaliwa kuwa la nadra kwa sababu katika matukio ya huko nyuma ambayo Baraza ilichunguza daima yalihusisha mamlaka dhidi ya waandishi.

Tukio hilo la Songea lilikuwa ni la kipekee kutokana na ukweli kwamba waandishi wa habari walidaiwa kufanya mambo kama kundi la mbweha kumshambulia mwandishi mwenzao ambaye walidaiwa pia kumtenga na kumuita muongo kutokana na taarifa zake. Zaidi ya hayo, mwandishi huyo alitoa taarifa kwamba alikuwa anafuatiliwa na watu wenye kutia mashaka na wasiojulikana popote alipokuwa akienda, na usiku mmoja, alisikia sauti ngeni nje ya nyumba yake.

Ili kufika kwenye mzizi wa suala hilo, timu ya uchunguzi ya MCT iliwahoji waandishi saba wa Songea akiwemo mlalamikaji, Geofrey Nilahi. Vile vile ilizungumza na viongozi wa mkoa pamoja na wilaya.

Waandishi wengine waliohojiwa ni pamoja na: Andrew Kuchonjoma – Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Ruvuma, Amon Mtega kutoka gazeti la Mtanzania, Joseph Mwambije kutoka ITV, Mawazo Mwaijenga kutoka Azam TV, Joyce Joliga wa MCL na Crencesia Kapinga ambaye anafanyia kazi gazeti la Majira.

Timu ya uchunguzi ya MCT pia ilifanya mahojiano na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Christina Mndeme, Mkuu wa Wilaya ya Songea Pololet Mgema na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea Rajabu Mtiula. Timu hiyo pia ilifanya mahojiano ya simu na Diwani mmoja aliyejitambulisha kama Manfred Nzuyu.

Baadaye ilibainika kwamba Geofrey Nilahi alifanya hivyo baada ya kudokezwa na Simon Kapinga, Diwani wa Muhukuru Rilahi. Mwandishi huyo baadaye alitembelea vijiji vya Mipeta na Lunyele mnamo Septemba 26, 2018, na kuandika kuhusu hali mbaya ya shule kwenye Kata ya Muhukuru. Taarifa yake iliyochapishwa ilitoka kwenye gazeti la 'Tanzania Daima' mnamo Oktoba 4, 2018 chini ya kichwa cha habari: 'Kamwelwe, Ndalichako na Ummy wanajua madudu haya?'

Jinsi habari hiyo ilivyochukuliwa na wahariri wa Tanzania Daima, ikiwa na picha za mawaziri wahusika wa afya, elimu na miundombinu bila kauli zozote kutoka kwao ilikuwa chonganishi na kuhusishwa na uhasimu wa kisiasa unaoendelea mjini Songea. Ilitafsiriwa na timu ya MCT kama ilivyo kwa msemo wa kutia 'chumvi kwenye kidonda.'

Habari nyingine ilirushwa na kituo cha televisheni cha Channel 10 mnamo Oktoba 14, 2018. Habari hizo ziliambatana na picha zinazoonyesha wanafunzi walionyong'onyea waliokaa juu ya matofali kwenye darasa moja lililoezekwa kwa nyasi. Vile vile zilionyesha picha za watembea kwa miguu wakivuka daraja moja lililotengenezwa kwa miti iliyopinda linaloning'inia likiwa katika hali ya hatari. Wananchi walikuwa hawaruhusiwi kutumia daraja binafsi lililopo pembeni yake lililo katika hali nzuri ambalo lilikuwa linamilikiwa na kanisa moja la hapo.

Habari hizo ambazo ziliwakasirisha na kupelekea uongozi wa wilaya na mkoa kuchukua hatua zilikuwa hazikidhi vigezo kiweledi kwani zilikuwa hazina vyanzo vya kutosha na mamlaka hazikupewa haki ya kujibu.

Kutokana na mahojiano yaliyofanywa na Timu ya uchunguzi, kilichopelekea hasa kuchukuliwa kwa hatua hiyo ni hasira za viongozi kutokana na kuwepo kipande cha mkanda wa video iliyowekwa kwenye mitandao ya kijamii huku ikisindikizwa na wimbo maarufu wa propaganda ya CCM uitwao: 'Mtaisoma Namba,' ambao unaweza kuchukuliwa kama kejeli kwa wapinzani wa kisiasa kuhusiana na kusonga mbele kwa msafara wa CCM katika siasa za ushindani. Kwenye tukio hili wimbo huo ulionekana kuwakejeli wapiga kura wa Mbunge wa Peramiho kwamba badala ya kuendeleza jimbo hilo mwanamama huyo alikuwa amefanya kinyume na matarajio.

Nilahi alikiri kuandika habari hizo lakini alikana kuhusika na propaganda hizo zilizowekwa mitandaoni. Hata hivyo, viongozi wa kisiasa mkoani humo wanamlaumu mwandishi huyo (Nilahi) kuhusika na uwekaji wa propaganda hizo kwenye mitandao ya kijamii.

Rajabu Mtiula, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea alinukuu msemo wa Kiswahili wa 'aliyekutwa na ngozi', akimaanisha kwamba '…aliyekutwa na ngozi ya mnyama wa wizi lazima ndiye mwizi.'

Habari hizo zilitafsiriwa kulenga kuonyesha kwamba Mbunge wa Peramiho wa hivi sasa, Waziri Jenister Mhagama, alikuwa ameshindwa kutekeleza ahadi za maendeleo kwenye jimbo lake likiwa halina chochote isipokuwa shule zilizochakaa, huduma mbovu za afya na madaraja hatarishi ya muda.

Jitihada za Nilahi kuweka uwiano kwenye taarifa zake kwa kupata mitazamo ya viongozi wa wilaya na mkoa hazikufanikiwa kwa vile walimpuuza na kumchukulia kama mtu anayetumika kisiasa kuuchafua uongozi wa mkoa wa Ruvuma.

Pamoja na yote, jambo moja ni dhahiri: habari za Nilahi, pamoja na kukosa uwiano, zilichochea kuchukuliwa kwa hatua kutoka kwa viongozi wa wilaya na mkoa ambao katika nyakati tofauti walitembelea maeneo yaliyoelezewa kuwa na changamoto za kimiundombinu na kijamii.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Songea iliitisha mkutano maalumu kujadili na kushughulikia taarifa zilizotolewa kwenye vyombo vya habari.

Timu hiyo ya MCT pia ilifanya mahojiano na waandishi wa habari waliokuwa wametembelea maeneo hayo, wakiambatana na viongozi wa wilaya, mkoa na mbunge wa eneo hilo. Baadhi ya waandishi hao hawakuweza kupinga usahihi wa taarifa za Nilahi.

Kutokana na ziara hiyo, baadhi ya waandishi waliripoti juu ya matumizi mabaya ya fedha za ujenzi wa kituo cha afya cha kijiji. Wengine waliripoti kwamba daraja binafsi lililopo jirani na eneo hilo sasa lilikuwa wazi kutumika tu wakati wa mchana na usiku kukiwa na dharura.

Wakati nchi ikikaribia Uchaguzi Mkuu wa 2020, kuna mtazamo kwamba wanasiasa mbalimbali wanaowania nafasi za ubunge wanatumia vyombo vya habari kuwafanya mahasimu wao waonekane hawafai. Hali hiyo ndiyo iliyopelekea Nilahi kuchukuliwa kwamba alikuwa anatumiwa na watu wanaowania Jimbo la Peramiho, kitu ambacho mwandishi huyo anakikana. Kulikuwepo pia na taarifa zisizothibitishwa kwamba mbunge huyo wa sasa alikuwa ametumia shilingi milioni sita kuwalipa waandishi kuandika habari chanya kumhusu.

Christina Mndeme, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, alieleza kutofurahishwa kwake na habari hizo na kusema mwandishi huyo asingezirusha au kuziandika bila kuomba majibu kutoka kwa mamlaka husika. Mkuu huyo wa mkoa aliongeza kusema kwamba yeye mwenyewe binafsi anamjua Nilahi na kusema kwamba mamlaka mkoani humo zina uhusiano mzuri wa kikazi na waandishi.

Pololet Mgema, Mkuu wa Wilaya ya Songea, alilalamika kuhusiana na kutokuwepo kwa uwiano kwenye habari hizo za mwandishi huyo. Aliomba vyombo vya habari kuwawezesha kifedha waandishi wao ili waweze kufuatilia habari kikamilifu kuepuka kutegemea tu vyanzo vya habari.

Kutokana na maelezo ya viongozi wa wilaya na mkoa waliohojiwa, madarasa hayo ya nyasi yaliyoripotiwa hayapo kabisa. Kitu ambacho mwandishi huyo aliweza kuwa alikiona, walisisitiza, ni shule zisizo rasmi zilizoanzishwa na jamii za wahamiaji, na zinajulikana kama 'shule shikizi'. Kutokana na hitaji kubwa la elimu kwa watoto, mara nyingi mamlaka hulazimika kuzitambua 'shule' hizo na kuzipatia walimu.

Viongozi wa eneo hilo pia walimshutumu Nilahi kutengeneza mazingira ya picha za wanafunzi hao wakiwa ndani ya darasa moja la nyasi. Viongozi hao walidai kwamba mwandishi huyo alipanga wanafunzi hao kutolewa kwenye jengo la darasa rasmi na kupelekwa kwenye chumba kimoja cha nyasi ambacho kinatumika kama jiko na ukumbi wa chakula.


Maelezo mengine ni kwamba mara tu baada ya habari hiyo kutoka, darasa hilo la nyasi liliungua moto katika harakati za kuondoa ushahidi wa kuwepo kwake.

Manfred Nzuyu, Diwani wa Kata ya Muhukuru, ambaye alielezewa kuwa chanzo cha taarifa hizo, alimruka kabisa mwandishi huyo wakati wa mkutano maalumu wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

## 6.0 TAARIFA ZA WAHUSIKA MMOJA MMOJA:

### 6.1 Andrew Kuchonjoma: Mwenyekiti Klabu ya Waandishi wa Habari Ruvuma (RPC):

Kuchonjoma alikuwa wa kwanza kuhojiwa na timu ya uchunguzi ya MCT. Alitoa maelezo ya jumla ya hali ilivyokuwa kabla ya timu hiyo kwenda kwa wahojiwa wengine ikiwa ni pamoja na Geofrey Nilahi. Alisema alikuwa na majadiliano ya kina na Nilahi kufuatia tukio hilo. Alithibitisha kwamba ni kweli mwenzake huyo alikwenda Muhukuru kukusanya habari hiyo.



*Andrew Kuchonjoma*

Kwa mujibu wa Kuchonjoma, baada ya Nilahi kuwa ameshakusanya taarifa hiyo, alijaribu kuweka uwiano lakini hakupata ushirikiano wa kutosha. Alisema Nilahi alikwenda kumuona Mkuu wa Mkoa Mndeme kwa kupata

upande wa pili wa mamlaka. Hata hivyo, mkuu huyo wa mkoa alimshauri kwenda kumuona mkuu wa wilaya. Wakati kipande cha mkanda wa video kiliporushwa kwenye mitandao ya kijamii na kusambaa, Nilahi alikutana na mkuu huyo wa wilaya, mkuu wa mkoa na mkurugenzi wa halmashauri. Kuchonjoma alisema kuna mtu mmoja asiyejulikana alisambaza kipande hicho kwenye mitandao ya kijamii. Hakuna anayeweza kutoa ushahidi wa wazi kama Nilahi ndiye aliyerusha kipande hicho cha mkanda wa video kwenye mitandao, japokuwa ndani yake kina vitu ambavyo alivikusanya kutoka Muhukuru.

Mnamo Oktoba 19 au 20, kikao maalum cha Halmashauri kiliitishwa kwa ajili ya kujadili taarifa hiyo lakini madiwani na viongozi wote wa kata walikanusha taarifa hizo zilizomo kwenye habari za Nilahi na kwenye mitandao ya kijamii. Kwa mujibu wake, Halmashauri iliwachagua waandishi watano kukanusha taarifa ya Nilahi. Waandishi hao ni:

1- Cresencia Kapinga – Majira

2- Mawazo Mwaijenga – Azam TV

3- Amon Mtega – Mtanzania

4- Joseph Mwambije – ITV

5- Joyce Joliga – magazeti ya MCL

Waandishi hao waliochaguliwa walipelekwa kwenye maeneo ambayo Nilahi alisema alipata habari hizo. Hata hivyo, hawakufika sehemu ambapo picha za darasa hilo lililoezekwa kwa nyasi zilipigwa.

Katika ushuhuda wake, Kuchonjoma alisema kwamba baadhi ya waandishi walikuwa wanatumia majukwaa ya mitandao ya kijamii kumshutumu Nilahi kwamba 'alitengeneza' picha hizo za darasa lililoezekwa kwa nyasi "Waandishi wote waliosafiri na viongozi wa kisiasa kutembelea sehemu ambazo Nilahi alikusanya habari zake walitoa taarifa ambazo zilikuwa zinapingana na zile za Nilahi," Kuchonjoma alisema.

Habari na kipande cha mkanda wa video cha Nilahi viliibua hali ya kurushiana maneno makali kwenye kundi la mtandao wa WhatsApp wa Klabu ya Waandishi wa Habari ya Ruvuma. Ilibainika kwamba waandishi wawili, Joyce Joliga wa MCL na Cresencia Kapinga wa Majira wana uhusiano wa karibu na Waziri Mhagama. Vile vile, Kapinga ni Diwani wa Ndilima.

Kuchonjoma alisema tatizo kubwa kwenye kipande hicho cha video kilikuwa ni kuunganishwa kwa wimbo wa propaganda wa CCM na sio maudhui ya msingi yaliyomo. Kwa mujibu wa Kuchonjoma, Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema, alimtishia Nilahi kumchukulia hatua mahakamani.

Kuchonjoma alisema mara nyingi alikuwa anamshauri Nilahi umuhimu wa kufuata maadili ya kazi ya uandishi wa habari, daima akimuelezea umuhimu wa kuhakikisha kuwepo usawa na uwiano kabla ya uchapishaji.

Pia, kuna taarifa kwamba ofisa mmoja wa chama cha CCM aliyetambulika kama Lazaro Bunungu, anashirikiana na Nilahi kusambaza habari za kumpunguzia umaarufu Waziri Mhagama. Bunungu anasemekana kuwania jimbo la Peramiho kwenye chaguzi za mwaka 2020. Hata hivyo, taarifa hizo hazikuweza kuthibitika.
Maoni yake kuhusu tabia na udhaifu wa waandishi mkoani Ruvuma:

1. Tamaa:
2. Kupuuza maadili ya kitaaluma;
3. Kujiingiza katika mahusiano ya karibu na wanasiasa na
4. Kufanya mambo kinyume na weledi.

### 6.2 Geofrey Nilahi: Mwandishi wa kujitegemea wa Channel 10 na 'Tanzania Daima':



***Geofrey Nilahi***

Nilahi, mwanachama wa Klabu ya Waandishi wa Habari ya Ruvuma (RPC), alikuwa ni mtu wa pili kuhojiwa na timu ya MCT. Kwa mujibu wake, alifuatilia habari hiyo baada ya kudokezwa na Simon Kapinga, Diwani wa Muhukuru Rilahi.

Kapinga alimueleza Nilahi kuhusu kufungwa kwa Shule ya Msingi ya Muungano, kutokana na ukosefu wa walimu.

Mwandishi huyo alisema mara ya kwanza alifahamishwa juu ya shule hiyo wakati alipokuwa akifuatilia habari isiyo husiana na hiyo huko Muhukuru Rilahi.

Baada ya kudokezwa, Nilahi alikwenda kwenye eneo hilo mnamo Septemba 25, 2018. Hata hivyo, awali, hakuweza kusafiri kwenda huko kwa sababu ya kuwa porini na umbali mrefu kutoka Songea Mjini. Vile vile alikuwa hana fedha ya nauli. Baadaye aliwasiliana na diwani mwingine aliyetambuliwa kama Manfred Nzuyu (Kata ya Muhukuru), ambaye alijitolea kumsaidia kwa kupeleka pikipiki imchukue hadi Muungano.

Akiwa njiani kuelekea Muungano, Nilahi alifika Kata ya Kizuka ambapo aliona jengo moja lililoezekwa na nyasi na wanafunzi wakicheza nje. Hiyo ilikuwa ni Shule ya Msingi Ulamboni, alisema. Hata hivyo, hiyo haikuwa shule aliyokuwa anaikusudia. Lakini, alisimamana kupiga baadhi ya picha za video. Hakukuwepo na walimu shuleni hapo na Nilahi aliungana na wanafunzi hao waliochangamka kwenye eneo la shule hiyo.

Manne kati ya majengo ya madarasa kwenye shule hiyo yalijengwa kwa juhudi za wakazi wa eneo hilo. Baadhi ya madarasa yalikuwa na madawati lakini kwenye mengine, matofali yalikuwa yametumika kama samani za darasani kutokana na ukosefu wa madawati. Hapakuwepo na ubao wa ukutani.

Vile vile alimhoji Mwenyekiti wa Kijiji cha Ulamboni kuhusiana na juhudi za pamoja kijamii kutengeneza vitu ambavyo havikuwepo.

Kiongozi huyo pia alimfahamisha juu ya kiongozi mmoja wa kijiji ambaye alikimbia na fedha ambazo zilikuwa zimechangwa na wananchi kwa ajili ya ujenzi wa zahanati. Kutokana na kukosekana kwa zahanati hiyo, wakazi wa Ulamboni wanalazimika kuvuka Mto Ruvuma kupitia daraja lisiloaminika la mbao lenye urefu wa mita 150. Manfred Nzuyu alimpeleka Nilahi kuona daraja hilo.

Nilahi alilala siku hiyo nyumbani kwa Nzuyu. Siku iliyofuata, waliendelea na safari hadi Shule ya Msingi ya Muungano, ambayo ndiyo Nilahi alikuwa ameikusudia. Akiwa shuleni hapo, alikutana na wanafunzi takriban 20. Aliieleza timu ya uchunguzi kwamba aliamini kuwa kuna mtu aliwaambia wanafunzi hao kufika shuleni hapo siku hiyo.

Nilahi aliwahoji baadhi ya wanafunzi, mwalimu mmoja wa kujitolea, Mtendaji wa Kata (Rajab Issa), Diwani wa Kata (Nzuyu), Mwenyekiti wa Kamati ya Shule na baadhi ya wanajamii. Aligundua kwamba kila siku wanafunzi walikuwa wanabeba matofali kwenda kukalia madarasani kama madawati. Vile vile walikuwa wanabeba mawe ambayo yanatumika kama chaki. Pia, wakati wa mvua, sehemu hiyo ilikuwa haiwezi kufikika.

Nilahi alitetea taarifa yake hiyo ambayo alisema ilikuwa imefanywa kitaalamu. Alisema alituma ujumbe mmoja mrefu wa simu kwa Jenista Mahagama, Mbunge wa Peramiho tarehe 26 Septemba, baada ya kukusanya taarifa zote hizo. Hata hivyo alidai Mbunge huyo hakuujibu ujumbe huo. Tarehe 27 Septemba, alituma ujumbe mwingine kwa mbunge huyo, akimkumbushia kuhusu ujumbe wake wa awali. Mwanamama huyo inadaiwa pia hakujibu.

Habari yake ya kwanza ilichapishwa Oktoba 4 kwenye gazeti la Tanzania Daima chini ya kichwa cha habari; 'Kamwelwe, Ndalichako, Ummy Mwalimu, mnayajua haya yanayotokea Ruvuma?'

Siku kumi baadaye, habari hiyo ilirushwa kwenye Televisheni ya Channel 10. Alisema mhariri wa makala wa Tanzania Daima Deo Mkuchu, hakumuuliza swali lolote kuhusiana na makala hiyo. Baada ya makala na habari hiyo kuchapishwa kwenye Tanzania Daima na kurushwa na Televisheni ya Channel 10, alikwenda kumuona Ofisa Mawasiliano kwenye ofisi za Halmashauri.

Nilahi alikiri kwamba hakuwahi kuwasiliana kupata kauli za Mkuu wa Mkoa Mndeme wala Mkuu wa Wilaya Mgema. Alikwenda kuonana na viongozi hao wawili baada ya habari yake kurushwa na kuchapishwa.

Siku tatu baada ya habari yake kurushwa kwenye Channel 10, iliiumbuka mitandaoni kipande cha mkanda wa video chenye maudhui kutoka kata za Kizuka na Muhukuru, kikichombezwa na muziki wa propaganda. Nilahi alikana yeye mwenyewe kuhusika na vipande hivyo vya mikanda ya wimbo wa propaganda wa CCM, japokuwa alikubali maudhui kuhusiana na shule, wanafunzi, madaraja na mahojiano vilikuwa vyake. Alisisitiza kwamba kuna mtu 'alichezea' sehemu ya

taarifa yake rasmi za video. Na yeyote aliyefanya hivyo, ndiye aliyeongezea wimbo wa propaganda wa CCM.

Nilahi alisema kwamba kwa sababu ya habari zake hizo, viongozi walitembelea maeneo husika wakiongozana na waandishi wa habari. Kwa mujibu wa Nilahi, waandishi hao walichukuliwa kwenda safari hizo kwa shabaha ya kukanusha habari zake. Nilahi alitoa mfano wa habari mojawapo ya kukanusha taarifa zake kuwa iliyorushwa kwenye Televisheni ya Azam, japokuwa hakuweza kukumbuka tarehe kamili ambayo ilirushwa.

Mnamo Oktoba 20, 2018, mkutano maalum wa halmashauri ya wilaya uliitishwa. Waandishi wengi walihudhuria kuripoti juu ya mkutano huo, lakini Nilahi hakualikwa. Kwa mujibu wa Nilahi, tangu habari hizo mbili na kipande hicho cha video viliposambaa, alikuwa haalikwi kwenye mikutano ya waandishi wa habari au matukio yoyote ya habari yaliyoandaliwa na serikali. Vile vile alisema baadhi ya wanataaluma wenzake walimshambulia kwenye mitandao ya kijamii na kumshutumu kutoa habari zisizo za kweli.

Tarehe 16 Oktoba, wakati akiwa kwenye pikipiki njiani kurudi nyumbani, gari moja ambalo ndani yake lilikuwa na watu wa kutilia mashaka lilimpita na kusimama mbele yake. Pia nyakati za usiku, siku mmoja kabla ya tarehe 15 Oktoba, alisikia sauti ngeni nje ya nyumba yake.

Vile vile, picha zote ambazo alipiga wakati alipokwenda Muhukuru zilitoweka kiutatanishi kwenye kompyuta yake binafsi. Na kwamba anaishi kwa hofu na ameshayaripoti matukio hayo kwa polisi.

### 6.3 Amon Mtega: Mwandishi anayeripoti kwa gazeti la 'Mtanzania':

Amon Mtega alianza kwa kuelezea kile ambacho alidhani timu ya uchunguzi ya MCT ilikuwa inahitaji kukijua kuhusiana na shule ambayo Nilahi aliripoti habari zake.



*Amon Mtega*

Alisema shule inayozungumziwa haikuwa shule iliyosajiliwa rasmi, lakini ilikuwa ni 'shule shikizi' iliyounganishwa kwenye shule moja rasmi.

Alisema shule kama hizo hazina walimu wenye sifa kamili, zinajengwa kupitia juhudi za kujitolea za jamii na wanafunzi wanasajiliwa kwenye shule rasmi ambazo zinaweza kuwa kwenye kata nyingine.

Mtega alisema kwamba kile alichofanya Nilahi kilikuwa ni kuvuta hisia za changamoto ambazo shule hizo zinakabiliwa nazo, bila kujali kwamba zilikuwa ni 'shule shikizi' au shule rasmi za umma.

Alisema daima kuna njia mbalimbali za uandishi wa habari. Baadhi ya waandishi wa habari wanaripoti habari za mafanikio tu na wengine wanakuwa na shauku juu ya changamoto tu. Katika kesi hiyo, Nilahi aliangazia kwenye changamoto. Mtega alisema baada ya video hiyo kusambaa, Mkuu wa Mkoa Mndeme aliwachukua yeye pamoja na waandishi wengine kuhakiki kama kile alichoripoti Nilahi kilikuwa kweli.

Waliporudi kutoka huko, Mtega aliandika habari chini ya kichwa cha habari: "Mkuu wa Mkoa apiga marufuku shule shikizi." Alisema mkuu huyo wa mkoa aliamini kwamba serikali haitaweza kuhudumia shule shikizi, kwa hiyo akaamua kuzisitisha. Hata hivyo, Mndeme alitoa amri kwa walimu, madawati na vifaa vingine vya shule kupelekwa kwenye shule hizo.

Alisema kwamba habari yake haikuwa imekusudia kukanusha au kupingana na kile ambacho Nilahi alikuwa amekichapisha na kukirusha hewani hapo awali, bali alikwenda tu kuripoti ziara ya Mkuu wa Mkoa kama ambavyo kila mwandishi angefanya.

Alisisitiza kwamba ziara hiyo ya Mkuu wa Mkoa haikuwa na nia ya kukanusha bali kuhakiki kile ambacho Nilahi alikuwa amekiripoti hapo awali.

"Hakuna yeyote anayeweza kukanusha habari ambayo imechapishwa na mwandishi mwingine, isipokuwa tu yule ambaye alikuwa ameripoti suala hilo," alisema Mtega.

Alisema kwamba wanasiasa wengi hawatumii Klabu ya Waandishi wa Habari ya Ruvuma kwa kwa ajili ya kusimamia matukio ya vyombo vya habari bali wanawasiliana tu na waandishi mmoja mmoja.

Alitaja baadhi ya waandishi waliofanya ziara hiyo na Mkuu wa Mkoa Mndeme:

1- Cresencia Kapinga – Majira
2- Mawazo Mwaijenga – Azam TV
3- Amon Mtega – Mtanzania
4- Joseph Mwambije – ITV
5- Joyce Joliga – MCL

Hata hivyo, alisema, mkuu huyo wa mkoa hakufika kwenye eneo ambapo shule ile ya nyasi ilipokuwa kutokana na umbali wake. Yeye anaamini kwamba Nilahi alikuwa sahihi na hakupanga chochote kwa sababu hakutakuwa na mantiki yoyote kufanya kitu kama hicho.

Akizungumza kuhusu kipande hicho cha picha ya video kwenye mitandao ya kijamii, Mtega alisema hana uhakika kama Nilahi ndiye aliyekitayarisha na kukisambaza. Hata hivyo, kwa sababu yeye ndiye aliyekuwa amekusanya maudhui hayo, kila mmoja anamnyooshea kidole. Hata hivyo, Mtega alisema, ilikuwa ni Nilahi ambaye aliingiza kipande hicho cha video hiyo yenye wimbo wa propaganda wa CCM katika kundi la *WhatsApp* la wanahabari.

Akijibu swali kama kulikuwepo na uhusiano wa kisiasa kwenye suala hilo, Mtega alisema kwamba baadhi ya masuala yana ushawishi wa kisiasa.

Aliweka wazi kwamba chanzo kimoja jijini Dar es Salaam kilimueleza kwamba baadhi ya waandishi walikuwa wamepokea zaidi ya shilingi milioni sita kukanusha habari hiyo ya Nilahi. Mtega alisema kwamba japokuwa Mhagama ni maarufu kwenye jimbo lake, bado mwanamama huyo anaweza kuwa na wasiwasi kuhusiana na chaguzi za mwaka 2020.

Alizidi kusema kwamba kumekuwepo na taarifa kwamba mwanasiasa mmoja ambaye hakutajwa alimlipa Nilahi kufuatilia taarifa hiyo. Mtega alisema kwamba anahisi mtu mmoja aitwaye Lazaro Bunungu ambaye anasemekana kuwania jimbo la Peramiho, angeweza kuwa anahusika na sakata hilo. Hata hivyo, wazo hilo halikuweza kuthibitika.

### 6.4 Joseph Mwambije: Mwandishi wa kujitegemea wa ITV:

Joseph Mwambije alianza kwa kusisitiza kwamba kulikuwa hakuna tatizo kwenye habari za Nilahi. "Habari hizo zilikuwa ni za kweli. Hata hivyo, kitu ambacho kilileta mkaganyiko na kuzusha mjadala ni kipande cha video ya wimbo wa CCM kikiambatanishwa na video ya Waziri Mhagama akiwa Bungeni," alisema.

Mwambije anafikiri ni kinyume cha maadili kwa mwandishi wa habari kupamba maudhui yake kwa propaganda za kisiasa. Hiyo inakuwa uharakati wa kisiasa, alisema. Mwambije alisema japokuwa hana uhakika kama Nilahi ndiye aliyetayarisha na kuvisambaza vipande hivyo vya video, ilikuwa ni kweli kwamba mwandishi huyo ndiye aliyekwenda kwenye eneo hilo na kuja na habari ambayo haikuwafurahisha baadhi ya watu.

Alisema habari hiyo ya Televisheni ya Channel 10 haikuwa na ukakasi kama kipande cha video ambacho kilisambaa kwenye mitandao ya kijamii.

Alipoulizwa kama alikwenda na mkuu wa mkoa kwenye vijiji hivyo ambavyo Nilahi aliviripoti, alisema kwamba yeye alialikwa pamoja na waandishi wengine. Hata hivyo, alisema, ziara hiyo ya Mkuu wa Mkoa Mndeme ilikuwa ni ya kawaida na sio ya kipekee au maalumu.

Mwambije alisema hakuwahi kuandika habari ya kukanusha habari ya Nilahi, badala yake aliweka msisitizo kwa kiongozi wa kijiji ambaye alikimbia na fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati.

Alisema aliibuka na habari ambayo alikuwa anaamini itavutia chombo chake cha habari kuendana na matakwa ya mhariri wake ambaye alikuwa ameshamuarifu.

Aliongeza kusema kwamba Waziri Mhagama, muda mfupi baadaye, alitembelea eneo hilo, lakini, alisema, hakuambatana naye kwa sababu alikuwa na majukumu mengine. Hata hivyo, alimtuma mpiga picha wake.

Mwambije alihudhuria mkutano maalum wa Halmashauri ya Wilaya tarehe Oktoba 20, 2018. Alisema wakati wa mkutano huo maalum wa Halmashauri, viongozi wote wa kata walikana kufanya kazi na Nilahi au hata kumpa ushirikiano wowote katika jithada zake za kupata habari ya kata za Muhukuru na Kizuka.

Alisema hajapokea maelekezo yoyote kutoka kwa Waziri Mhagama au Mkuu wa Mkoa Mndeme juu ya namna ya kuandika habari zake kuhusiana na suala hilo.

Mwambije, hata hivyo, alikiri walipokea shilingi 50,000 kila mmoja, ambazo, alisema, ilikuwa ni posho ya 'kawaida' kwa mwandishi.

Pamoja na migogoro na hali ya kutoelewana iliyotokea, Mwambije alisema habari za Nilahi zilikuwa nzuri kwa sababu ziliwaamsha viongozi hao kushughulikia changamoto zinazovikabili vijiji hivyo. "Lakini sikufurahishwa na kipande hicho cha video chenye wimbo wa CCM ndani yake," aliongeza.

Mwambije alisema sakata lote hilo limegubikwa na mihemko ya kisiasa. Alimgusia mtu mmoja, Lazaro Bunungu kuhusika na sakata hilo. Bunungu anasemekana kuonyesha nia ya kuwania jimbo la Peramiho.

Alisema kwenye kundi lao la *WhatsApp*, kulikuwepo na mabishano yasiyofaa kati ya Nilahi na baadhi ya waandishi wenzake.

Mwambije alisema baadhi ya wanasiasa, (hakutaja jina) wamemtumia ujumbe wa simu wa kuwashuhumu waandishi wa habari wa Ruvuma kwa kukubali kutumiwa na wanasiasa.

Mwandishi huyo alidai alikuwa pia mhanga wakati fulani, pale alipofungiwa kuripoti chochote au hata kutembelea Nyasa baada ya kuandika habari juu ya changamoto za ardhi na maji kwenye eneo hilo.

"Wanasiasa wanakanusha chochote kile kinachoweza kuharibu harakati zao kisiasa au kupoteza nafasi zao," alisema.

Aliwataja waandishi waliohudhuria mkutano huo maalum wa Halmashauri kama:

1- Amon Mtega – Mtanzania
2- Grace Amlike – Key FM
3- Joseph Mwambije – ITV
4- Mawazo Mwaijenga – Azam TV

### 6.5 Mawazo Mwaijenga: Azam TV

Mwaijenga ambaye alidai kuwa rafiki wa Nilahi, na kuongeza kusema kwamba kwa kawaida hujadili taarifa zao na kubadilishana baadhi ya vidokezo vyaa habari. Kwa hiyo, aliieleza timu ya MCT, Nilahi alitaka ushauri wake kabla ya kipande hicho cha video kusambaa kwenye mitandao ya kijamii na hata kabla ya habari hizo kupelekwa kwenye vyombo vya habari anavyovifanyia kazi.



***Mawazo Mwaijenga:*** *Azam TV*

Alisema Nilahi alimuonyesha baadhi ya picha ghafi za video kutoka kwenye eneo hilo. Alisema baadhi ya video zilionyesha jengo hilo bovu la shule na daraja hilo hatarishi.

Mwaijenga aliieleza timu ya MCT kwamba alimshauri mwenzake huyo kutochapisha habari hizo hadi atakapopata kauli kutoka kwenye mamlaka husika. Mwaijenga alisema hakuiona habari ya Nilahi kwenye Televisheni ya Channel 10, lakini alikiona kipande cha video ambacho kilikuwa kinasambaa kwenye mitandao. Kipande hicho cha video kilikuwa na maudhui ambayo alikuwa ameyaona kwenye picha ghafi ya Nilahi, picha ambayo, hata hivyo, haikuwa na wimbo wa CCM.

Kwa mujibu wa Mwaijenga, kipande cha video cha Nilahi kilikuwa ni dokezo kwake na alitaka kutengeneza habari kutokana nacho. Alikwenda kumuona Mkuu wa Wilaya Pololet kutaka kauli yake kuhusiana na vipande hivyo vya picha za video ili aweze kufuatilia habari nyingine, lakini Mkuu huyo wa Wilaya alisema itakuwa vizuri zaidi kama watasafiri pamoja kwa vile yeye pia alikuwa na mipango ya kutembelea eneo hilo.

Mwaijenga alisema baada ya kuwasili, walikwenda moja kwa moja kwenye Shule ya Msingi Mipeta na walikuta kwamba haikuwa taasisi rasmi ya elimu bali shule shikizi. Alisema jengo ambalo liliripotiwa na Nilahi halikuwa darasa bali sehemu inayotumika kupikia uji. Mwaijenga aliwahoji baadhi ya walimu ambao, hata hivyo, hawakutoa "ushirikiano." Alisema vile vile aliwahoji baadhi ya wanakijiji.

Nia yake, alidai, ilikuwa ni kutumia habari ya Nilahi kama dokezo ambalo atalitumia kuja na habari nzuri zaidi. Hata hivyo, Mwaijenga alisema, baadaye aligundua kwamba kipande cha video cha Nilahi, sasa kikiwa na wimbo wa propaganda wa CCM, kilikuwa kinazunguka kwenye mitandao.

Alisema hakuweza kuwa na uhakika kama ilikuwa ni Nilahi ndiye aliyekitayarisha na kukiweka kwenye mitandao ya kijamii. Mwaijenga alisema baada ya ziara hiyo, habari yake ilichapishwa lakini hakuweza kukumbuka habari yake hiyo hasa iliegemea kwenye suala gani.

Baadaye, Mkuu wa Mkoa Mndeme alitembelea tena eneo hilo na wakati huo alialika kundi jingine la waandishi wa habari. Kwa mujibu wake, waandishi walioalikwa walikuwa wanatoka:

1. Jogoo FM;
2. Azam TV;
3. MCL;
4. 'Majira' na
5. 'Mtanzania'.

Alisema lengo la Mkuu huyo wa mkoa lilikuwa ni kukagua miradi ya maendeleo na changamoto kwenye eneo hilo. Kwa mujibu wa Mwaijenga, habari yake iliyorushwa hewani na Azam TV iliegemea kwenye amri ya Mkuu wa Mkoa Mndeme ya kuzuia uwepo wa shule shikizi.

Mwaijenga alisema kwamba takriban wiki mbili baada ya ziara hiyo ya mkuu wa mkoa, Waziri Mhagama alitembelea Muhukuru kuwashukuru wapigaji kura kwa kumchagua kiongozi mwingine wa kata kutoka CCM. Mwanamama huyo pia alitembelea shule zile ambazo hali zake ziliripotiwa na Nilahi.

Mwaijenga alisema kwamba baadaye, wanawake wa UWT waliandaa hafla ya kumtunikia Waziri Mhagama hadhi ya "Malkia wa Nguvu" wa Jimbo la Peramiho. Tukio hilo lilifanyika Mpitimbi.

Kufuatia kutunikiwa huko hadhi ya "Malkia Mhagama," kulikuwepo na taarifa kwamba Nilahi alitayarisha kipande kingine cha video, ambacho kinadaiwa kutaka kuonyesha kwamba hata wakati waziri huyo akipandishwa daraja mpaka hadhi ya malkia, wapigaji kura wake walikuwa bado wakiendelea kukabiliwa na changamoto kadhaa… Kipande hicho cha video kilionyesha tena daraja hilo na lile darasa la nyasi.

Mwaijenga alisema alikuwa hana uhakika kama Nilahi ndiye aliyetayarisha kipande hicho cha picha ya video. Hata hivyo, kilikuwa na baadhi ya maudhui ya picha zilizofahamika kama za kwake.

Mwaijenga anaamini kwamba kuna mgogoro wa siku nyingi kati ya Mhagama na Nilahi, japokuwa hakuna anayejua mzizi hasa wa mgogoro huo.

Mwaijenga alisema Nilahi alimkabili kwa kumuuliza ni kwanini aliandika habari ambazo zinapingana na zake na alijibu shutuma hiyo kwa kusema kwamba alichofanya ni kuripoti kile kilichotokea kwenye ziara.

Nilahi aliwapigia baadhi ya waandishi kwenye makao makuu ya Azam TV akihoji ni kwanini walirusha hewani habari za Mwaijenga ambazo zililenga kuleta mtazamo hasi kwa zile ambazo yeye (Nilahi) alikuwa ameshaziripoti awali.

Wakati alipoulizwa kama anamjua Lazaro Bunungu, Mwaijenga alisema alikuwa hamjui. Hata hivyo, alisema aliona ujumbe moja uliyorushwa kwenye mitandao ya kijamii na Bunungu ukiwatuhumu waandishi wanne kutoka Ruvuma kupokea shilingi milioni sita kutoka kwa mwanasiasa mmoja ambaye hakutajwa.

Alisema kwamba mara kadhaa Nilahi hurusha ujumbe mwingi wa kuudhi kwenye kundi la WhatsApp la Klabu ya Waandishi wa Habari ya Ruvuma.

### 6.6 Joyce Joliga: Mwandishi wa kujitegemea MCL:

Joyce Joliga alisema alikiona kipande cha habari cha Nilahi ambacho kilikuwa kinaishutumu vikali CCM, na kuongeza kwamba ofisa mmoja kutoka ofisi ya CCM mkoani Ruvuma alimuomba kumrushia kipande hicho.

Joliga alithibitisha kwamba Nilahi ndiye aliyetengeneza kipande hicho cha habari chenye wimbo wa propaganda wa CCM, 'Mtaisoma Namba' kikiambatanishwa na kipande cha Mheshimiwa Jenista Mhagama akiwa kwenye Mkutano wa Bunge na hali mbaya ya shule kwenye jimbo lake.




*Joyce Joliga*

Alipoulizwa kama aliandika habari yoyote ya kukanusha kile ambacho Nilahi alikuwa ameripoti, Joliga alisema: "Sijawahi kukanusha habari iliyoandikwa na Nilahi wala mwandishi mwingine yeyote Mkoani Ruvuma." Pia alikana kuwa rafiki wa Mheshimiwa Jenista Mhagama.

## 6.7 Cresensia Kapinga: Mwandishi wa kujitegemea wa gazeti la Majira

Cresensia Kapinga alisema alipata kipande cha habari cha Nilahi chenye wimbo wa CCM kutoka kwa mfanyabiashara mmoja aliyeko Songea Mjini.



*Cresensia Kapinga*

Kapinga alikana kuandika habari iliyolenga kukanusha habari ya Nilahi, na kuongeza kwamba yeye aliandika stori kwenye gazeti la 'Majira' ambayo ilichapishwa ikiwa na kichwa cha habari; "Jinsi Halmashauri ya Wilaya ya Songea ilivyosaidia shule shirikishi za Songea Vijijini".

Kapinga alidai kwamba waandishi wa habari mjini Songea wana matatizo, na kuongeza kwamba wengi wao wana tabia ya kufanyakazi kwa manufaa binafsi. Mwandishi huyo hakuweza kufafanua zaidi.

### 6.8 Christina Mndeme: Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

Timu ya watu watatu ya uchunguzi kutoka MCT iliomba kukutana na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme.

Wakati wa mkutano huo, Mndeme alilalamika kwamba waandishi wa habari mkoani humo walikuwa wamesikitishwa na taarifa ya Nilahi ambayo ililenga kuchafua taswira ya serikali na chama tawala CCM.

Alisema kipande hicho cha habari kwenye mitandao ya kijamii kilitengenezwa kwa lengo hasi, na kuongeza kwamba shule hizo shirikishi ambazo Nilahi alidai zilikuwa za nyasi, hazipo kabisa mkoani humo.

" Alichofanya Nilahi ni kuwachukua wanafunzi kutoka mahali fulani na kuwaomba wakae ndani ya kibanda kimoja cha nyasi ambacho kinatumika kupikia uji kwa ajili ya wanafunzi. Kwenye picha hizo ambazo zimepigwa na Nilahi, amekielezea kibanda hicho kama darasa, kitu ambacho sio kweli," alisema mkuu huyo wa mkoa.



***Christina Mndeme:*** *Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma*

Yote hayo, alisema Mkuu huyo wa mkoa, yalikusudia kuchafua taswira ya viongozi wa serikali ya Mkoa wa Ruvuma, akiwemo Mbunge wa Peramiho, Jenista Mhagama.

Mndeme alisema baada ya vipande hivyo vya habari kurushwa hewani, Nilahi alikwenda ofisini kwake na kuomba msamaha.

Mkuu huyo wa mkoa alisema mwandishi huyo alidai kwamba Diwani wa eneo hilo alikuwa amemuomba kupiga "picha za kupotosha" kama njia ya kuishinikiza serikali kusaidia miradi ya maendeleo kwenye eneo hilo, ikiwemo ujenzi wa shule.

"Nilahi alikiri kwamba habari yake kwenye kipande hicho cha habari ilikuwa haina uwiano kwa sababu hakutafuta maoni yoyote kutoka kwa viongozi wa serikali mkoani humo, lakini alikana kuchomeka wimbo huo wa CCM 'Mtaisoma Namba' kwenye vipande vyake hivyo vya habari. Nilahi pia alikiri kwamba yeye ni kada wa CCM, sasa ni kwanini alichapisha habari yake kwenye gazeti linalomilikiwa na upinzani (Tanzania Daima)?" alihoji mkuu huyo wa mkoa.

Mkuu huyo wa mkoa alisema Nilahi alikiri kwamba alituma makala yake 'Tanzania Daima,' japokuwa alikuwa mwepesi kueleza kwamba ni wahariri waliopo Dar es Salaam ndiyo waliochagua picha ambazo ziliambatana na habari hiyo.

"Kile alichofanya Nilahi ni sawa na kuwavua nguo viongozi wa Mkoa wa Ruvuma mbele ya umma," alisema, na kuongeza kwamba mamlaka za mkoa zilimuuliza Nilahi kama kulikuwepo wanasiasa wowote nyuma ya habari hizo hasi. Hata hivyo, mwandishi huyo alikana kufanya kazi kwa matakwa ya mwanasiasa au wanasiasa wowote wakati huu nchi ikielekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2020.

Mndeme alieleza masikitiko yake kwa MCT, akisema pamoja na mafanikio ya serikali, kulikuwepo na watu wachache waliolenga kuchafua taswira yake.

Mwanamama huyo alisema ni kweli kwamba kulikuwepo na changamoto zinazoikabili serikali, lakini ilikuwa ikifanya kazi kwa bidii kuzipatia ufumbuzi changamoto hizo.

Mkuu huyo wa mkoa aliahidi kwamba mamlaka mkoani humo zitaendelea kufanyakazi kwa karibu na Klabu ya Waandishi wa Habari wa Ruvuma na wanachama wake. "Baada ya vipande hivyo vya habari, nilimuelekeza Mkuu wa Wilaya ya Songea kutembelea maeneo hayo ambayo yalielezewa kwenye habari za Nilahi kufanya tathmini ya hali ilivyo sehemu yenyewe, lakini hatukumwalika mwandishi huyo kuambatana na mkuu wa wilaya kwa sababu hatukufurahishwa na kile alichokuwa amefanya," alisema Mndeme.

### 6.9 Pololet Kamando Mgema: Mkuu wa Wilaya ya Songea

Mkuu wa Wilaya ya Songea Pololet Kamando Mgema alikiri kwamba changamoto kwenye uandishi wa habari zilikuwa haziwezi kuepukika. Alisema kushindwa kuweka uwiano kwenye habari ilikuwa ni miongoni mwa matatizo yanayoikabili taaluma hiyo.


*Pololet Kamando Mgema*

Alisema kwamba Wilaya ya Songea ilikuwa na bahati ya kuwa na idadi nzuri ya waandishi wakiwakilisha karibu vyombo vyote vya habari nchini Tanzania.

Hata hivyo, alisema Mgema, kipande cha habari ambacho kilihusishwa na Nilahi kilikuwa 'kimechezewa' na kwa hiyo hakiwezi kutumika kama picha ya hali halisi ya sehemu ambayo picha hizo zilipigwa.

Hata hivyo, alisema, kufichua hali mbaya kwenye maeneo ya vijijini sio kitu kibaya; cha muhimu ilikuwa ni jinsi habari hiyo ilivyowasilishwa.

Mkuu huyo wa wilaya alikiri kwamba ilikuwa kweli ujenzi kwenye shule shirikishi kwenye maeneo yanayokaliwa na wakulima wahamiaji kutoka Wilaya ya Mbinga ulikuwa bado unaendelea, lakini alisema hakukuwepo shule zilizoezekwa kwa nyasi kama vipande hivyo vya habari vya Nilahi vilivyoonyesha.

Vile vile alikiri kwamba kwa vile ukusanyaji wa mapato wilayani humo ulikuwa ni wa chini, kumekuwepo na bajeti ndogo ya kuboresha shule shirikishi zinazojulikana pia kama shule za pembezoni.

Pamoja na hayo, Mgema alidai, Nilahi alifadhiliwa na Diwani wa Muhukuru Manfred Nzuyu kwa nia ya kushinikiza serikali kutoa pesa kwa ajili ya kufanyia maboresho shule na zahanati kwenye eneo lake.

Alisema Mbunge wa Peramiho Jenista Mhagama alitoa mabati na saruji kwa ajili ya ujenzi wa shule kwenye sehemu kubwa ya eneo hilo lenye wakulima wahamiaji. Alibainisha kuwa maeneo haya yanakabiliwa na uharibifu kutokana na ukataji miti katika kusafisha ardhi kwa ajili ya kilimo.

Kwa mtazamo wake, mamlaka mkoani humo hazina chuki dhidi ya Nilahi na hapaswi kujihisi kutengwa. Aliomba kwa MCT kuhakikisha vyombo vya habari vinaboresha maslahi ya waandishi kama njia ya kuwalinda dhidi ya kutumiwa na watu .wenye malengo binafsi

### 6.10 Rajab Mtiula: Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea:



*Rajab Mtiula*

Baada ya kupata taarifa kuhusu kipande cha video cha Geofrey Nilahi, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea Rajab Mtiula alisema aliitisha mkutano maalum wa Halmashauri ya Wilaya tarehe 20, Oktoba 2018.

Mkutano huo uliitishwa baada ya kubaini kwamba Nilahi hakutafuta jibu kutoka aidha kwa Mtiula au Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Songea kuhusiana na yale aliyoyagundua Songea Vijijini.

Mtiula alisema wakati alipowasiliana na Madiwani wa maeneo ambayo Nilahi alikuwa ameyatembelea, walikana kufanya mazungumzo na mwandishi huyo kuhusiana na shule ambazo zipo kwenye hali mbaya.

Kwa mfano, alisema Mtiula, wakati Nilahi alipokutana na Diwani wa Muhukuru, Manfred Nzuyu, walizungumza kuhusiana na michango ya wanakijiji kwa ajili ya ujenzi wa zahanati, kupotea kwa fedha zilizokusanywa na ujenzi wa daraja.

"Madiwani wote kutoka kwenye maeneo yaliyotembelewa na Nilahi walikana kumpatia malazi," alisema Mtiula. Aliongeza kusema kwamba wakati wa mkutano huo wa wajumbe 23 ambao ni Madiwani , baadhi walipendekeza kwamba Nilahi afanyiwe uchunguzi wa akili na uhakiki wa sifa zake za uandishi wa habari.

Alisema mkutano huo wa Halmashauri uliamua kuwaomba Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma ma Mkuu wa Wilaya ya Songea kuchukua hatua za kurekebisha na kuhakikisha kwamba kile alichofanya Nilahi hakitatokea tena.

Alipoulizwa kama Halmashauri hiyo ilipokea mrejesho wowote kuhusiana na maombi yao kama ilivyoelezwa kwenye maamuzi yao, Mtiula alisema alikuwa hana taarifa zozote kuhusiana na hilo.

Aliongeza kusema kwamba Halmashauri hiyo pia ilitoa wito kwa waandishi wa habari Mkoani Ruvuma kufuata maadili ya kitaaluma, ikiwemo haja ya kuweka uwiano kwenye stori ili kuepuka migongano.

### 6.11 Manfred Nzuyu: Diwani wa Muhukuru:

Timu ya uchunguzi ya MCT ilizungumza na Diwani wa Muhukuru, Manfred Nzuyu, kupitia simu yake ya mkononi. Diwani huyo alisema alikuwa haoni tatizo kuhusiana na juhudi za Nilahi za kuibua changamoto ambazo zinaiathiri kata yake.

Alisema ni kweli kwamba wanakijiji kwenye eneo hilo chini ya himaya yake hawana zahanati na wanalazimika kutembea kilomita kadhaa au kutumia pikipiki kufikia kituo cha afya kilicho jirani.

Nzuyu alitanabainisha kwamba kwa wanakijiji hao kupata huduma za afya, wanalazimika kuvuka Mto Ruvuma, lakini bado hakuna daraja salama.

Alisema stori za Nilahi zilichochea hatua za kuwepo mabadiliko. Mara tu baada ya taarifa zake, kulikuwepo na majadiliano kati ya Mkuu wa Mkoa Mndeme na watendaji wa misheni ya jirani kuwaruhusu wanakijiji kutumia daraja hilo linalotumiwa na seminari.

Alisema ni kweli kwamba Shule ya Msingi ya Runyele ilifungwa kwa sababu ya ukosefu wa walimu. Nzuyu pia alisema alihudhuria mkutano maalum wa Halmashauri ambao uliitishwa Oktoba 20, 2018.

Alisema mkutano huo ulijadili mahususi kipande cha habari za Nilahi. Alisema, mada ilikuwa juu ya kipande hicho cha video kikionyesha daraja bovu la mbao zilizopinda, darasa lililoezekwa kwa nyasi na kipande cha video kilichoambatanishwa na wimbo wa propaganda wa CCM. Nzuyu alisema kipande hicho chenye wimbo wa CCM kilimuudhi kila kiongozi wa Ruvuma, akiwemo yeye mwenyewe.

Alisema mkutano huo wa Halmashauri uliitishwa mahususi kukanusha taarifa ya Nilahi na kipande hicho cha video chenye wimbo huo wa propaganda wa CCM. Nzuyu pia alisema Nilahi alipomtafuta baada ya mkutano wa Halmashauri, alimshutumu mwandishi huyo kuhusiana na kipande hicho cha video.

Zaidi ya hayo, Nzuyu alitanabaisha, Nilahi alichanganya taarifa. Diwani huyo alisema kibanda hicho cha nyasi kilichopo Kata ya Kizuka kilielezewa kuwa katika Kata ya Muhukuru. Changamoto huko Muhukuru, Nzuyu aliieleza timu ya MCT, ilikuwa ni shule moja isiyo na walimu na daraja hilo bovu la mbao.

Diwani huyo alikiri kufanyakazi na Nilahi na hata kutuma pikipiki kumchukua kutoka Muhukuru. Alieleza kwamba alimpatia mwandishi huyo msaada wowote aliohitaji kwa sababu alikuwa anaamini taarifa ya vyombo vya habari ingeweza kuongeza kasi ya kushinikiza upatikanaji wa mabadiliko muhimu katika kata yake.

## 7.0 HITIMISHO

7.1 Viongozi wa Mkoa wa Ruvuma na Wilaya ya Songea walihamaki kwa kupitiliza katika kushughulikia habari zilizotolewa na Nilahi.

7.2 Hapakuwa na haja ya uongozi mzima kuhamaki kiasi hicho dhidi ya habari hizo hasi na kutuma ziara mfululizo za ujumbe kwenye maeneo yaliyobainishwa kuwa na changamoto katika kujaribu kusafisha kile kilichoitwa hali ya hewa iliyochafuka.

7.3 Viongozi wangeshughulikia jambo hilo bila mihemuko, kwa umakini badala ya kufanya pupa kwa hisia za kuogopa mamlaka za kitaifa kama walivyobainisha katika majibu yao.

7.4 Halmashauri ya Wilaya ya Songea ilihamaki katika kuitisha mkutano maalumu kwa shabaha tu ya kumsulubu mwandishi huyo kufuatia habari zake hizo zilizotoka.

7.5 Uitishaji wa mkutano huo maalumu ilikuwa ni sawa na 'kutumia nyundo kuua nzi' na yalikuwa ni matumizi mabaya ya pesa adimu za umma.

7.6 Viongozi katika ngazi zote za ofisi za umma wanapaswa kuwa na ngozi ngumu katika kushughulikia masuala yanayowaweka bayana kwa ajili ya kutathminiwa na wananchi.

7.7 Kama taarifa juu ya changamoto za maendeleo katika eneo fulani inawalazimu viongozi kuitisha mkutano wa dharura wa halmashauri na ziara mfululizo za viongozi kwenda eneo husika, je uongozi wa aina hii utachukua hatua gani kama likitokea janga kubwa?

7.8 Ukweli kwamba hatua za makusudi zilichukuliwa kumtenga mwandishi Geofrey Nilahi kwa kutomshirikisha matukio yoyote baada ya kutolewa habari zake kuhusu changamoto za maendeleo wilayani Songea, na ukweli kwamba polisi walipuuza madai yake kwamba alikuwa anafuatiliwa na watu wasiojulikana, ni uthibitisho kwamba alikuwa anatishiwa kiusalama.

Na hata wakati tunaandaa taarifa hii, kulikuwa na madai kwamba Nilahi alikuwa anafuatiliwa na polisi.

7.9 Waandishi waliruhusu wenyewe kutumiwa na viongozi dhidi ya mwandishi mwenzao. Jambo hili linawekwa bayana na ukweli kwamba katika ziara zote zilizofanyika kwenye maeneo husika ambako mwandishi huyo ndiye aliyetoa habari kwa mara ya kwanza kuhusu changamoto zilizopo katika vijiji husika, aliachwa na hakualikwa hata kwenye kikao maalumu cha Halmashauri ya Wilaya.

7.10 Ilikuwa siyo sahihi kwa waandishi kukubali fadhila kutoka kwa wanasiasa, viongozi na makundi mengine yenye maslahi yao, kuonesha taswira chanya au yenye mafanikio na upotoshaji halisia.

7.11 Waandishi waligawanyika kutokana na ama utashi wao kisiasa au maslahi banafsi.

7.12 Kwa sababu kuweka uwiano na kuhusisha vyanzo vingi ni muhimu katika habari, mwandishi alifanya makosa kutoona mapungufu hayo mara ya kwanza alipotoa habari zihusizo changamoto za maendeleo.

7.13 Taarifa zilzotolewa zinaonesha kwamba mwandishi alishindwa kutoegemea upande wowote na kwa hivyo kutozingatia dhana ya kutofungamana na upande wowote katika kazi zake. Jambo hili pia linahusisha wahariri kama wasimamizi wa mwisho wa vyombo vya habari ambao hutoa taarifa zenye mapungufu makubwa kiweledi.

7.14 Ilikuwa sio sahihi kuchanganya kazi, habari au makala na propaganda za siasa kama ilivyofanywa kwa kushirikisha wimbo wa CCM, 'Mtaisoma Namba.' Kuchanganya habari hiyo na wimbo wa propaganda bila shaka kulileta hali ya kutoaminiwa kwa mwandishi aliyetoa taarifa za changamoto za maendeleo Peramiho ambayo iliunganishwa na kipande kilichozunguka katika mitandao muda mfupi baada ya habari yake kuchapishwa katika gazeti la Tanzania Daima na kurushwa katika televisheni ya Channel 10.

# 8.0 MAPENDEKEZO:

8.1 Viongozi katika ngazi zote - taifa, mkoa na wilaya - wanapaswa kushughulikia kwa uangalifu taarifa za vyombo vya habari.

8.2 Viongozi wanapaswa kuwa watulivu na kuepuka taharuki wakutanapo na taarifa hasi za vyombo vya habari.

8.3 Wafanyapo kazi na waandishi wa habari na vyombo vya habari kwa ujumla, viongozi wasisukumwe na uoga wa jambo lisilojulikana au uoga wa kuchukuliwa hatua kali za kinidhamu na uongozi wa kitaifa.

8.4 Viongozi katika ngazi zote wanapaswa kujijengea uwezo wa kushughulika na kukabiliana na taarifa za vyombo vya habari. Hili haijalishi nyadhifa zao na athari ya taarifa hizo za vyombo vya habari.

8.5 Viongozi wanapaswa kuitikia maombi ya waandishi kupata taarifa kama muhimu na hatua makini katika kufanikisha utekelezaji wa Sheria ya Uhuru wa Kupata Taarifa ya mwaka 2016.

8.6 Waandishi wakatae kutumiwa kufanikisha malengo binafsi ya watu au vikundi dhidi ya waandishi wenzao.

8.7 Waandishi wanapaswa kukataa kurubuniwa a wanasiasa, viongozi au makundi mengine yenye maslahi, wanapaswa kugoma kutumiwa kuonyesha taswira za uongo kuwa kweli au uhalisia hasi.

8.8 Maslahi ya kisiasa au binasfi hayapaswi kupewa nafasi na taaluma ya uandishi.

8.9 Ni jambo la muhimu na lazima kuwepo na uwiano katika habari na pia kuwepo na vyanzo kadhaa katika taarifa.

8.10 Wahariri kama watu wa mwisho katika utoaji wa habari kupitia vyombo, wanapaswa kuwa makini katika kufuata misingi ya taaluma, sheria na taratibu na kuhakikisha kwamba habari zinazochapishwa au kurushwa hewani zinakidhi vigezo vya maadili.

8.11 Kazi za uandishi - taarifa, habari au makala - hazipaswi kuchanganywa na propaganda za kisiasa.

8.12 Waandishi wa habari wanaofanya kazi hiyo kwa wakati uliopo hawapaswi kuwa na nafasi katika vyama vya siasa ili kuwa huru katika kufanya kazi zao kama wasimamizi katika jamii.

8.13 Matatizo au kutokuelewana miongoni mwa waandishi kama mfano huu wa Nilahi dhidi ya waandishi wenzake wilayani Songea, vinapaswa kushughulikiwa haraka na taasisi kama MCT na Umoja wa Klabu za Waandishi Tanzania (UTPC).

8.14 Vyombo vya habari vinapaswa kuboresha maslahi ya wawakilishi wao mikoani na kuwalipa kwa wakati ili kuondoa utegemezi wa vyanzo vya habari na makundi mengine yenye maslahi.

8.15 Menejimenti za vyombo vya habari zijenge mazoea ya kutembelea wawakilishi wao mikoani mara kwa mara ili kupata uhalisia wa mazingira ya kazi na kufanya jitihada za kuyaboresha.

8.16 MCT inatakiwa kuendeleza ziara katika vyombo vya habari na kukutana na waandishi pamoja na menejimenti ili kupata changamoto za kitaaluma wanazopata na kushughulikia mapendekezo ya ya uboreshaji na ushauri wa namna ya kusonga mbele.



12 TanzaniaDaima JAMII JUMAMOSI JUNI 23, 2018

JUMAMOSI JUNI 23, 2018 JAMII TanzaniaDaima 13

# Balaa la fedha za miradi kwa viongozi, watendaji Ruvuma

>>Songea, Mbinga, Namtumbo, Madaba, Mbinga Mji, Tunduru na Nyasa wapigana vikumbo wao kwa wao

NA GEOFREY NILAHI

daimanews@yahoo.com



10 TanzaniaDaima UCHUMI & BIASHARA

# Kamwelwe, Ndalichako na Ummy wanajua madudu haya ya Songea?

*Inatoka uk 9*

Mhukuru.

Kwa adha wanayo pata wananchi hao ni namna ya kuvuka kwenda kituo cha Afya Kalembo kutokana na kuwepo kwa mto mkubwa wa Ruvuma ambapo wananchi walijenga daraja la miti lenye urefu wa mita 150 na upana mita moja na nusu.

S.L.P.843,
**SONGEA- RUVUMA.**

MOBILE.0766085373
Email.nilahij@gmail.com

KATIBU RUVUMA PRESS CLUB,
S.L.P 843,
**SONGEA-RUVUMA.**

Received 16/10/2018

RUVUMA PRESS CLUB BOX 843 SONGEA

**TAARIFA YA KAULI YENYE VITISHO NA VIASHIRIA VYA HATARI KUTOKA KWA VIONGOZI DHIDI YANGU.**

Husika na mada tajwa hapo juu,mwenye jina na anuani tajwa ni mwandishi wa habari ninayeripotia Channel Ten na mwandishi wa Makala za uchunguzi katika gazeti la Tanzania daima,kutoka katika mkoa wa Ruvuma.

Katika ufuatiliaji wa habari za uchunguzi nikiangazia maisha ya wananchi wa vijijini,Septemba 10.2018 nilitembelea kijiji cha Magwamila kata ya Mhukuru Lilahi wilaya ya Songea mkoani Ruvuma,nilikutana na changamoto zinazo wakabili wananchi hakuna barabara ya kupita gari,nilikuta zahanati imefungwa waganga walikuwa wameondoka kwa kipindi kirefu.

Niliandika habari iliyorushwa Channel Ten na Makala ya gazeti iliyochapishwa septemba 15 mwaka huu,iliyopewa kichwa cha habari ''BORA USIKIE YA KUAMBIWA SIO UYAONE YA MAGWAMILA''na makala ya uchumi gazeti la septemba 29 iliyokuwa na kichwa cha habari ''UMASIKINI WATESA WATU MAZAO YAKIOZEA NDANI''

Septemba 26 nilitembelea kata ya Mhukuru katika kijiji cha Mipeta na Lunyele,baada ya kupata taarifa ya kufungwa kwa shule ya msingi Muungano kwa sababu ya kukosa walimu,ninakutana na changamoto nyingine nyingi zinazoathili huduma ya afya,elimu pamoja na ukosefu wa miundombinu ya barabara na madaraja.

SONGEA?''Nendeni kijiji cha Mipeta,Lunyele na Malambo'' na taarifa ya ... shule yenye madarasa ya nyasi,utoro wa walimu pamoja na kufungwa kwa shule ilirushwa Channel ten.

Taarifa hizi zimetikisa viongozi wa mkoa na taifa na kuwa gumzo katika mitandao mbalimbali za kijamii hali iliyosababisha viongozi katika ngazi hizo kwenda katika maeneo yote yaliyotajwa ili kujiridhisha na kile nilichoripoti.

Niliitwa na mkuu wa mkoa Christina Mndeme na kufanya mazungumzo tukiwa wawili ofisini kwake nanukuu sehemu ya mazungumzo''nimeambiwa na mwenyekiti wa ccm taifa niandike maelezo ya kutosha kwa nini nakidharirisha chama cha mapinduzi,hapa nilipo sina uhakika kama nitabaki salama,nikifukuzwa kazi mimi wewe itakusaidia nini,basi Rais akuteue wewe uje ukalie kiti hiki''

Nilijitahidi kunyamaza ili nimpe nafasi aeleze alichonacho rohoni,hatimaye nilijieleza na kuweka wazi kila kilichotokea,viongozi wa mkoa na wilaya wanadai kuwa nina lengo la kumchafua mbunge,kwa kuwa nimeripoti mabaya na kuacha mazuri aliyofanya mbunge.

Nikiwa kwenye maeneo yote ya vijiji niliweza kuwasiliana na mbunge Jenista Mhagama kwa sms nikimweleza kila changamoto nilizo ziona nikimuomba akipata nafasi tuongee lakini hakuna msg aliyowahi kujibu.

Nilienda kwa mkuu wa wilaya Pololeti Mgema kwenda kusikiliza kauli ya serikali baada ya habari kuandikwa nilishambuliwa kwa maneno alikataa kurekodiwa wala kupigwa picha kwa madai kuwa mimi nimewachukua wanafunzi na kwenda kuwakalisha kwenye mabanda ya nyasi.

Shule hiyo wameikataa na kudai kuwa sio ya serikali ni yawananchi ingawa ina mwalimu wa serikali,nanukuu sehemu ya maneno yake''Wewe umetimiza dhamira yako serikali yote imechafuka sio wilaya mkoa wala taifa,mimi mwenyewe hapa nilipo sijui kama mambo haya yatapita salama umetuvuruga,nataka kujua ni nani aliyekutuma,mimi naipenda kazi yangu ikiharibika nashughulika na wewe''

Nilinyamaza na baadae nikamwambia toka mwanzo wa safari hadi mwisho mpaka mawasiliano yangu na mbunge hata hivyo anaukubali ukweli lakini bado anadai kuwa nina nia ya kuwachafua kwa kuwa yapo mazuri ambayo sikuandika.

Wametumiwa waandishi wengine wa habari kwenda kukanusha habari nilizoripoti,waandishi hao wamekuwa wakinitukana kwenye magroup na inbox wakinituhumu kuwa ni mwongo,baadhi ya jumbe nimeziprinti.

HATUA ZILIZO CHUKULIWA NA SERIKALI BAADA YA HABARI KUENEA.

Nimewasiliana na mwenyekiti wa kitongoji cha ulamboni amesema kuwa madarasa ya nyasi katika shule ya Ulamboni yamechomwa moto watoto wanasomea juani ili kupoteza ushahidi,Halmashauri imepewa siku 14 wawe wameezeka vyumba vine vilivyojengwa na wananchi katika shule hiyo,wamepelekwa walimu wawili katika shule ya msingi iliyofungwa,daraja lililokuwa linahatarisha maisha ya wananchi katika mto Ruvuma limefungwa TARULA wamepewa siku 14 wawe wamejenga.

HALI YA USALAMA WANGU.

Toka tarehe 7,8,9 na 10 nyumbani kwangu usiku wa manane kuna watu wanazunguka nyumba hali inayo nipa wasiwasi na mashaka juu ya kinachoendelea,tarehe 9 saa tatu usiku kwenye barabara ya kuelekea nyumbani kwangu Ruhuwiko Songea nilikuta gari imepaki njiani pembeni kuna watu watatu baada ya mimi kupita nikiwa kwa bodaboda nilisikia wakisema washa gari wakaanza kutufuata nyuma kwa kasi nika mwambia dereva boda apite njia ambayo gari haiwezi kupita.

Nikashuka sehemu ya giza na kukaa katika nyumba moja isiyokaliwa watu kwa muda wa dakika 20 hivi baadae nikaenda nyumbani nikalala salama kwa mazingira yaliyopo nalazimika kutoka nyumbani mpaka mambo yatakapo tulia.

Naomba kuwasilisha.

……………………………………………

**GEOFREY NILAHI.**
**MWANDISHI WA HABARI CHANNEL TEN SONGEA.**

Fwd Photo from Geoffrey Nilahi

From: media@mct.or.tz
Sent: Friday, October 12, 2018 8:17 AM
To: Pili Mtambalike; Paul Mallimbo; hmtuy@mct.or.tz
Subject: Fwd: Photo from Geoffrey Nilahi
Attachments: IMG-20181008-WA0098.jpg

-------- Original Message --------
Subject: Fwd: Photo from Geoffrey Nilahi
Date: 2018-10-11 20:02
From: Geofrey Nilahi <jonilahi2015@gmail.com>
To: media@mct.or.tz

Ziara ya mh.waziri wa nchi,Sera,bunge,kazi,vijana,ajira ,ulemavu Jenista Mhagama kata ya Peramiho.??????amazing

---

Fwd picha.kufungwa kwa zahanati

From: media@mct.or.tz
Sent: Friday, October 12, 2018 8:21 AM
To: Paul Mallimbo; Kajubi Mukajanga; Pili Mtambalike; hmtuy@mct.or.tz
Subject: Fwd: picha.kufungwa kwa zahanati

-------- Original Message --------
Subject: Fwd: picha.kufungwa kwa zahanati
Date: 2018-10-11 20:17
From: Geofrey Nilahi <jonilahi2015@gmail.com>
To: media@mct.or.tz

ZAHANATI YAFUNGWA KWA UKOSEFU WA WAGANGA.mp4 [1]

Links:
------
[1]
https://drive.google.com/file/d/15nBszypuygVR7jBL9d5Ow76A_wIDTjDv/view?usp=drive_web

Fwd Screen sgort

From: media@mct.or.tz
Sent: Friday, October 12, 2018 8:16 AM
To: Pili Mtambalike; Paul Mallimbo; Kajubi Mukajanga; hmtuy@mct.or.tz
Cc: Ziada Kilobo
Subject: Fwd: Screen sgort

-------- Original Message --------
Subject: Fwd: Screen sgort
Date: 2018-10-11 20:00
From: Geofrey Nilahi <jonilahi2015@gmail.com>
To: media@mct.or.tz

Yajayo yanafurahisha,kumbe ulamboni ni mkondo wa shule ya msingi Kizuka na sio milambo ??????,Lunyele nako ni mkondo wa shule ya msingi Matama na sio shule ya msingi kwani zote hazijasajiliwa bado tuwe makini??????. Mbunge kote kachangia mabati na saruji pamoja na fedha taslim na ndio maana aliitwa kuweka jiwe la msingi kutokana na mchango wake wa vifaa vya viwandani.

---

Fwd Screen short.

From: media@mct.or.tz
Sent: Friday, October 12, 2018 8:19 AM
To: Pili Mtambalike; Paul Mallimbo; Kajubi Mukajanga; hmtuy@mct.or.tz
Subject: Fwd: Screen short.

-------- Original Message --------
Subject: Fwd: Screen short.
Date: 2018-10-11 20:11
From: Geofrey Nilahi <jonilahi2015@gmail.com>
To: media@mct.or.tz

[10/8, 20:19] Geoffrey Nilahi: Mbona manyasi hujaonesha ukweli haufichiki

[10/8, 20:19] KELE: Na bado??????

[10/8, 20:20] Geoffrey Nilahi: Huo sio uandishi any way fanyeni kazi.

[10/8, 20:23] KELE: Wewe kwa uandishi gani ulionao wa kupotosha jamii?

[10/8, 20:24] KELE: Manyasi sijaona zaidi ya kibanda cha kupikia kande za wanafunzi??

[10/8, 20:25] Geoffrey Nilahi: Naona akili yako imefika mwisho.

NILIAMUA KUBLOCK MSG ZAKE ZISIINGIE KWANGU.

Fwd VITISHO VINAVYOHATARISHA USALAMA

From: media@mct.or.tz
Sent: Friday, October 12, 2018 8:15 AM
To: Pili Mtambalike; Paul Mallimbo; Kajubi Mukajanga; hmtuy@mct.or.tz
Subject: Fwd: VITISHO VINAVYOHATARISHA USALAMA
Attachments: 5.jpg; 3.jpg; 1.jpg; 2.jpg

-------- Original Message --------
Subject: VITISHO VINAVYOHATARISHA USALAMA
Date: 2018-10-11 19:58
From: Geofrey Nilahi <jonilahi2015@gmail.com>
To: media@mct.or.tz

GEOFREY PETER NILAHI,

C/O RUVUMA

PRESS CLUB

PO.BOX

143,SONGEA,

MOBILE.0766085373,

Email.jonilahi2015@gmail.com

12/10/2018

KATIBU MTENDAJI,

BARAZA LA HABARI TANZANIA,

DAR ES SALAAM.

TAARIFA YA KAULI YENYE VITISHO NA VIASHIRIA VYA HATARI KUTOKA KWA VIONGOZI DHIDI YANGU.

Katika ufuatiliaji wa habari za vijijini,Septemba 10.2018 nilitembelea kijiji cha Magwamila kata ya Mhukuru Lilahi wilaya ya Songea mkoani Ruvuma,

Nilikutana na changamoto zinazo wakabili wananchi Ikiwa ni pamoja na ukosefu wa barabara,kufungwa kwa zahanati kwa kipindi kirefu.

Septemba 26 nilitembelea kata ya Mhukuru katika kijiji cha Mipeta na

Page 1

```
                                    Fwd VITISHO
From:   media@mct.or.tz
Sent:   Friday, October 12, 2018 8:18 AM
To:     Paul Mallimbo; Pili Mtambalike; Kajubi Mukajanga; hmtuy@mct.or.tz
Subject:        Fwd: VITISHO



-------- Original Message --------
Subject: VITISHO
Date: 2018-10-11 20:07
 From: Geofrey Nilahi <jonilahi2015@gmail.com>
To: media@mct.or.tz

Nimetuma email baadhi ya msg nilizokuwa natumiwa na waandishi wa habari
waliokuwa wametumiwa kukanusha story zangu,Yupo mwandishi Joyce Joliga
anajitambulisha kama yeye ni barozi wa mct nasikitika kusema kuwa kila
tunapopata matatizo anageuza mtaji wa kujipatia fedha.

niliwahi kupigwa ofisini kwa DE Samandito Gombo wa Mbinga na nikafikishwa
Polisi yeye alinitukana sana kwa msg

GEOFREY NILAHI SONGEA
```

**KIREFU:**

MCT – Baraza la Habari Tanzania

RC – Mkuu wa Mkoa

DC – Mkuu wa Wilaya

MP – Mbunge

RPC – Klabu ya Wanahabari wa Ruvuma

UTPC- Umoja wa Vilabu vya Wanahabari Tanzania

OCD - Mkuu wa Polisi Wilaya

ISBN 978-9987-710-75-1

MEDIA COUNCIL OF TANZANIA

**Kimetolewa na:**
**Baraza la Habari Tanzania (MCT)**
**S. L. P. 10160, Dar es Salaam, Tanzania.**
Simu: **+255 22 27757228 /2771947**
Baruapepe: **media@mct.or.tz**
Tovuti: **www.mct.or.tz**